TANGAZO LA SERIKALI NA. 912 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA USAFI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Rorya.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa;

"chanzo cha maji" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Vyanzo vya Maji;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rorya;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"kizimba cha taka" maana yake ni kizimba cha taka au

chombo maalum kilichowekwa na Halmashauri kwa ajili ya jamii kuhifadhia taka ngumu kabla ya kuzisafirishwa hadi kwenye jalala kuu lililoidhinishwa na Halmashauri;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko ndani ya Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"maji taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka ngumu" Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi anayeishi au anayemiliki eneo la nyumba, kiwanja au biashara kuhakikisha kwamba:

(a) mazingira yanayozunguka eneo lake yanakuwa safi wakati wote;

(b) taka zote zinakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri;

(c) anachimba shimo la kutupia taka litakalokuwa na urefu usiopungua kimo cha futi tatu na upana usiopungua futi mbili;

(d) anajenga choo imara cha kudumu kwa matofali na kuezeka kwa bati, tembe, majani, vigae chenye mlango unaofunga na kufunguka na kuhakikisha kwamba choo kinatumika wakati wote na kuwe na chombo cha maji tiririka na sabuni ya kunawa mikono;

(e) eneo lake halina mazalia ya mbu, panya na wadudu wengine hatarishi;

(f) maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama bila kujali yametoka kwenye chanzo

gani cha maji.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya aya ngodo ya (1) atakuwa ametenda kosa.

Uhifadhi wa maji taka

5.-(1)Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara anatakiwa:
kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhia maji taka;
kunyonya maji taka kila wakati karo linapojaa; na
kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote ambayo haijatenmgwa kwa ajili ya kuhifadhia maji taka.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya aya ndogo ya (1) atakuwa ametenda kosa.

Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

6. Mtu yeyote anayetengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa:

(a) kutimiza masharti na kanuni za afya; na
(b) kuwa na kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri.

Upimaji wa afya

7.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, mgahawa, baa, nyumba ya kulala wageni, bucha, muoka mikate au mtu anayeshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa kuhakikisha kwamba anapima afya yake kila baada ya miezi sita.

(2) Mmiliki yeyote wa biashara ya chakula atakayeruhusu mhudumu wake kufanya kazi bila kupimwa afya yake atawajibika kulipa faini isiyozidi elfu hamsini.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

8.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote ndani ya Halmashauri wakati wa kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa tisa na nusu

alasiri kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(2) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kushauri au kuelekeza watu au mtu kutokuishi katika jengo ambalo linahatarisha afya au maisha ya watu na viumbe hai.

(3) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuzuia shughuli mbalimbali wakati wa mlipuko wa ugonjwa ikiwa pamoja na kukamata vyombo au vifaa vingine vinavyotumika na ambavyo vinaweza kuleta madhara kwa wakazi wa Halmashari.

(4) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kufunga au kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Vifaa vya kuhifadhia taka ngumu

9.-(1) Kila mmliki wa jengo la makazi au mpangaji wa jengo la makazi au mtu yeyote anayefanyia biashara katika eneo lolote ndani ya Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhia takataka chenye mfuniko na atawajibika kukusanya takataka hizo kwenye vizimba vya kuzolea takataka katika maeneo yaliyoainishwa.

(2) Kila mmiliki wa jengo au mpangaji wa nyumba iliyoko katika ukanda wa kijani, katika maeneo ambayo hayajapimwa atalazimika kuwa na shimo kubwa la kukusanyia taka ngumu katika eneo lake.

Ada ya uzoaji taka

10. Halmashauri itawajibika kukusanya taka ngumu kutoka katika vizimba vya takataka vilivyoainishwa katika kila kata, na wazalishaji takataka watalipia ada au ushuru wa ukusanyaji wa takataka kama ilivyooneshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Ukusanyaji taka ngumu

11.-(1) Hairuhusiwi kuweka uchafu wenye asili ya maji maji kwenye pipa au chombo chochote cha taka ngumu au kitu chochote kinachoweza kulipuka na

kusababisha madhara.

(2) Taka ngumu zote zitakazokusanywa kwenye pipa au chombo cha taka zitabaki kuwa mali ya mkazi au mmliki wa eneo lile mpaka zitakapokuwa zimefikishwa kwenye kizimba cha taka au zitakapokuwa zimetolewa na Wakala kutoka katika eneo lake.

(3) Hairuhusiwi mtu yeyote kuchoma au kufukia taka ngumu bila kibali cha Halmashauri.

Eneo la kutupa Takataka

12. Halmashauri itakuwa na wajibu wa:

(a) kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia takataka;
(b) kuweka vyombo maalum vya kutunzia takataka katika maeneo ya Halmashauri; na
(c) kutoa huduma ya uzoaji takataka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa takataka hadi kwenye dampo.

Wajibu wa Mmiliki wa duka la kuuza nyama

13. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama kuhakikisha kwamba:

(a) ana jengo la kudumu lililosakafiwa na kuwekwa marumaru nyeupe kwenye sakafu na kuta kwa urefu wa futi sita kutoka usawa wa sakafu;
(b) jengo lina maji safi, gogo na misumeno ya kukatia nyama;
(c) kuna pipa la kuhifadhia takataka;
(d) mhudumu ana koti jeupe pamoja na viatu vyeupe aina ya buti;
(e) mhudumu anapima afya kila baada ya miezi sita.

Siku ya usafi

14.-(1) Kila jumamosi ya wiki ya pili na jumamosi ya wiki ya mwisho wa mwezi itakuwa ni siku maalamu ya kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yote ya

Halmashauri.

(2) Itakuwa ni wajibu na lazima kwa kila mkazi katika Kijiji na Kitongoji kushiriki usafi wa mazingira kwa siku iliyopangwa na Halmashauri katika maeneo yao na maeneo ya umma.

(3) Kila mtu atahakikisha eneo lake la makazi na linalomzunguka, eneo analofanyia biashara, eneo la wazi lililo karibu naye kwa umbali wa mita kumi na eneo la mazingira ya ofisi ni safi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Vikundi vya usafi

15. Halmashauri itahamasisha uundaji wa vikundi jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika Vijiji na Vitongoji baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Marufuku

16. Ni marufuku:

(a) mtu yeyote kuendesha biashara ya upulizaji dawa au biashara ya kuua wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni kutoka Halmashauri;

(b) mfanyabiashara yeyote kupanga bidhaa nje ya jengo lake la biashara, barabarani, vichochoroni au katika eneo lolote ambalo halikuidhinishwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(c) mfugaji kuruhusu mfugo au mifugo kuzurura ovyo mitaani au barabarani;

(d) mtu yeyote kutupa takataka za aina yoyote barabarani au eneo lolote la wazi, kwenye vichochoro au kwenye chanzo chochote cha maji au katika eneo lolote ambalo halijatengwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(e) mtu yeyote aliye ndani ya gari kudondosha taka

ngumu nje ya gari likiwa ndani au nje ya kituo cha magari na sehemu yoyote ambapo gari hilo linapita;

(f) mtu yeyote kuanzisha shughuli za kiwanda au mradi wowote unaoweza kuathiri mazingira bila kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

(g) mtu yeyote kuzuia maji kupitia njia yake ya asili kwa kujenga, kulima au kuweka kitu chochote kwenye njia ya maji kitakachoingilia mtiririko wa asili wa maji katika chanzo cha maji;

(h) mtu yeyote kuweka kitu chochote kwenye maji taka ambacho kinaweza kuathiri mtu yeyote au kuharibu mfumo wa tiba ya maji taka au kusababisha kuzuia mtiririko wa maji taka;

(i) mtu yeyote kulima kilimo cha matuta yanayosababisha maji kutuama ndani ya eneo la katikati ya mji;

(j) mtu yeyote kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo kwenye maeneo ya Halmashauri bila kibali;

(k) mtu yeyote kuegesha gari bovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi, barabarani na kusababidha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo;

(l) mtu yeyote kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika eneo lisilokuwa machinjio au duka la kuuza nyama au katika eneo lisiloruhusiwa na Halmashauri.

Makosa

17.-(1) Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hii kwa mtu yeyote:

(a) kujenga choo umbali usiozidi mita sitini kutoka kisimani, bwawani, mtoni au chanzo cha maji

yanayotumika kwa matumizi ya binadamu;

(b) kutoa kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, taka maji yenye kinyesi kutoka kwenye choo chake au bafu lake au karo la kuoshea vyombo au nguo au kutoka kwenye bomba lolote linalochukua taka maji na kuyatitirisha kwenye barabara, mtaa, mfereji wa maji ya mvua au mfereji wowote uliowazi;

(c) kutupa taka au kusababisha mtu mwingine atupe taka mahali popote pasiporuhusiwa na Halmashauri;

(d) kuuza chakula katika eneo ambalo halijatengwa au kusajiliwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(e) kuzika maiti katika eneo ambalo halikuainishwa kwa shughuli hiyo bila taarifa maalum kwa Afisa Mwidhiniwa;

(f) kutolipa ada ya takataka;

(g) kutembeza chakula mtaani bila kibali cha Halmashauri;

(h) kuchezesha michezo au kuonesha michezo au burudani katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;

(i) kuegesha gari bovu na kuliacha kando ya barabara au kichochoroni au eneo la wazi ambalo halijaidhinishwa kwa shughuli za gereji na kuliacha zaidi ya siku moja;

(j) kulima kandokando au ndani ya mita sitini kutoka kwenye chanzo cha maji;

(k) kutokuwa na pipa au chombo cha takataka chenye mfuniko katika eneo la biashara;

(l) kutokuwa na choo au kukutwa na choo kibovu au kilichojaa;

(m) kukutwa na shimo la taka maji lililojaa au ambalo halina mfuniko;

(n) kuziba kichochoro; au

(o) kutokuwa na chombo maalum cha kukusanyia

takataka ndani ya gari la abiria.

Adhabu

18. Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi elfu hamsini na isiyozidi Shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

19. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 10)*

ADA YA KUZOA TAKA

| Na. | Eneo | Kiasi cha Ada kwa Shilingi |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za kuisha au makazi kwa kaya, wauzaji wa mitumba, mbogamboga na nafaka | 24,000/= kwa Mwaka |
| 2 | Maduka ya Rejareja, Baa, Grosari, Wachoma chips, Kuku, Nyamachoma, saluni, Mamalishe, Sonara, mafundi nguo, wachoraji, studio, waosha magari, maduka ya kuuza dawa za binadamu, maduka ya kuuza dawa za mifugo na kilimo, klabu ya muziki wa usiku, vibanda vya wakala au ofisi za mabasi, masoko kwa chumba au meza, wauza bidhaa katika magari | 96,000/= kwa Mwaka |
| 3 | Mgahawa | 120,000/= kwa Mwaka |
| 4 | Nyumba za kulala wageni, Hoteli za Kitalii wauza mbao au karakana za kuranda mbao, gereji, duka la jumla, vituo vya mafuta | 144,000/= kwa Mwaka |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 19)*

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi; ………………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya; ……………………………………..……. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya RORYA, kwamba mnamo tarehe;…… ya Mwezi;….…. Mwaka; ……..… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya: ….… cha Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ya Mwaka 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU:

Leo tarehe:…....... ya mwezi:………… mwaka:…………..
Jina:…………………………………..…………………….
Saini:………………………..……………………………
MBELE YANGU :
Jin;…………………………….………..……………………
Cheo; …………………………………………………..…….
Saini; …………………………………………………………
Tarehe; …………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Rorya imegongwa kwenye Kanuni hizi za Kudumu kufutia azimio lililotolewa kwenye kikao cha Baraza la Halmashauri kilichofanyika mnamo Tarehe 5 mwezi Agosti, Mwaka 2022

ABDUL O. MTAKA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Rorya*

GERALD S. NG'ONG'A
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Rorya*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*